



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO



## OFISI YA HAKIMILIKI TANZANIA

### TAARIFA KWA UMMA

### WITO KWA WATUMIAJI WA KAZI SANAA NA MAANDISHI

**Dar es Salaam - 13 Mei, 2026**

Ofisi ya Hakimiliki Tanzania (COSOTA) ni Taasisi ya Serikali iliyoanzishwa chini ya Sheria ya Hakimiliki na Hakishiriki Sura 218 Rekebu ya 2023, kwa mujibu wa Sheria hiyo COSOTA ina wajibu wa kulinda na kutetea haki mbalimbali za wabunifu kwa kusimamia masuala ya Hakimiliki na Hakishiriki.

Kwa mujibu wa kifungu cha 45 cha Sheria hiyo matumizi ya kazi za hakimiliki na hakishiriki kinyume na taratibu za kisheria ni kosa. Mtu atakayebainika kufanya kosa hilo Ofisi inaweza kumtoza faini isiyozidi shilingi milioni ishirini (20,000,000) au kifungo kisichozidi miaka mitano, au vyote kwa pamoja.

Hivyo ili kuepuka migogoro isiyo ya lazima COSOTA inatoa wito kwa wadau wote wa kazi za wabunifu ikiwemo vyombo vya habari na mitandao ya kijamii kuhakikisha kuwa kazi wanazotumia kwenye vyombo vyao zina vyeti vya uthibitisho wa umiliki wa kazi (Copyright Clearance Certificate) kutoka COSOTA na kuhakikisha kuwa matumizi yoyote yanafanyika kwa ridhaa ya mmiliki au kwa leseni halali.

Aidha, COSOTA inatoa wito kwa wabunifu wote kusajili kazi zao kwani usajili ni hatua muhimu ya kuimarisha ulinzi wa kazi zao na kutoa uthibitisho wa umiliki. Vilevile kwa kazi zinazowasilishwa kwaajili ya usajili ni lazima zizingatie Mila, Desturi na Utamaduni wa Mtanzania, kinyume na hapo hazitasajiliwa.

Kwa pamoja tuendeleo kulinda na kuthamini ubunifu kama nguzo ya maendeleo ya kijamii na kiuchumi. Kwa ufafanuzi zaidi wasiliana nasi kupitia na namba ya simu **0738 015 014** au unaweza kutuma barua pepe kupitia [barua@cosota.go.tz](mailto:barua@cosota.go.tz).

Imetolewa na:

Anitha Jonas

**Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano kwa Umma**